

SUPA JACKPOT
1,010,689,585/-
KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA*150*87#



DAWA feki za nguvu za kiume, utoaji wa mimba zakamatwa

UKURASA 5



UKURASA 21

**NEYMAR
AITWA
CHELSEA**

Nipashhe

Alhamisi Juni 30, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580992

www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

CHADEMA YAONDOA KORTINI MAPINGAMIZI DHIDI KINA MDEE

UKURASA 3

Bunge laingilia michango shuleni


Waziri aelekezwa kurekebisha... *Ukurasa 2*



Pacha walioungana wenye umri wa miezi 9 ambao wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa kutenganishwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam kesho. Pacha hao walizaliwa wilayani Maswa mkoani Simiyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Saa sita za madaktari 31 kutenganisha pacha MNH

UKURASA 3



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (watatu kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela (wapili kushoto), wakikabidhi mfano wa hundi kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati), ikiwa ni sehemu ya gawio la serikali lililololewa na Benki ya CRDB, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. Wengine ni Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, David Silinde (wapili kulia), Naibu Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana, Patrobas Katambi (kulia), pamoja na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 5 NAPE: WANAHABARI BADO WANAKABILIWA NA MATATIZO

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema sekta ya habari nchini bado...



UKURASA WA 5 RC AAGIZA KUKAMATWA WALIOKULA FEDHA MBICHI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata watumishi...

Hukumu ya mchana hadi usiku yawapeleka jela viongozi CWT

UKURASA 2

MICHEZO

KOCHA MPYA SIMBA APEWA MASHARTI UK.23

MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza katika mkutano wa viongozi wa juu unaohusu kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa kwa kuunga mkono maendeleo endelevu ya uchumi wa buluu kwa nchi zinazoendelea, nchi zisizo na bahari pamoja nchi za visiwa vidogo. Mkutano huo ni sehemu ya mkutano wa viongozi wa juu ya uhifadhi wa bahari na rasilimali zake inayoendelea jijini Lisbon nchini Ureno jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

Bunge laingilia kati michango ya shule

Na Salome Kitomari, DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Musasa Zungu, amesema kuna kero kubwa ya michango shuleni inayowaumiza wananchi, akiitaka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuchukua hatua madhubuti.

Akiahirisha kikao cha jana cha Bunge jijini hapo, Zungu alisema wananchi wanabebeshwa mzigo wa michango ambayo inapaswa kulipwa na halmashauri zenye.

“Dodoma wameonyesha njia,

ninapongeza sana Halmashauri ya Dodoma, gharama za umeme, ulinzi zinafanywa na halmashauri,” alipongeza.

Zungu alisema kwa sasa kuna mtindo wa wazazi kulazimishwa kununua shuleni sare za shule, akibainisha kuwa kwa Dar es Salaam zinanunuliwa Karume ambako ni Sh. 5,000 lakini shuleni zikiuzwa Sh. 20,000.

“Hii michango na Waziri wa TAMISEMI uko hapa, hatuoni sababu kwanini halmashauri zisigharamie ulinzi, umeme. Kwanini wazazi wachangie ulinzi

na umeme? Mnaumiza wazazi sana kwa michango kama hii,” alisema.

Zungu alisema serikali imeondoa ada lakini bado kuna michango ya ziada inawasumbua wazazi, huku akitolea mfano wa nguo za michezo ambazo bei yake ni kubwa tofauti na uhalisia.

Naibu Spika huyo alimtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua za haraka juu ya suala hilo.

Juni 25 mwaka huu, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu kero ya michango kwa wanafun-

zi wanaoijiunga na kidato cha tano mwaka huu katika shule mbalimbali za Tanzania Bara.

Michango inayolalamikiwa inajumuisha gharama za ulinzi wa shule, wapishi wa shule, fedha za matibabu, tahadhari, ununuzi wa vitabu, michezo, gharama za mitihani na taaluma, kukodi godoro na ununuzi wa vifaa vingine vya shuleni.

Serikali imetangaza kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha, hakutakuwa na malipo ya ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, kama ilivyo kwa eli-

mumsingi (darasa la awali hadi kidato cha nne).

MAWAZIRI WATORO

Katika kikao cha jana, Zungu pia aliweka wazi kwamba mahudhurio ya wabunge bungeni hayaridhishi na kuwataka kuhakikisha wanakuwapo wakati wa kuahirisha Bunge leo.

“Kuna mbunge hayupo ndani ya Bunge na hayuko jimboni na wala taarifa kwa Spika hakuna, tunawaomba wabunge wote na mawaziri wawapo siku ya mwisho ya kufunga Bunge,” aliagiza.

Hukumu ya mchana hadi usiku yawapeleka jela viongozi CWT

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imetumia takriban saa saba kuwahukumu kifungo cha miezi sita gerezani Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Self (46) na Mwekahazina wa chama hicho, Abubakari Allawi.

Vilevile, katika hukumu hiyo yenye kurasa 122, mahakama imewataka washtakiwa hao kuirejeshea CWT Sh. 13,790,000 kwa madhara ambayo yametokea kwa sababu fedha zilizotumika ni mali ya chama hicho.

Hukumu hiyo ilisomwa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate kuanzia saa nane mchana hadi saa 2:30 usiku, akichambua kwa mapana hukumu yake iliyogusa pande zote mbili huku chumba cha mahakama kilichokuwa kimejaa ndugu, jamaa na marafiki wa washtakiwa hao kikiwa kimya.

Wakati hakimu akiendelea kuchambua hukumu yake, ili-potimu majira ya saa 10:39 jioni,

aliagiza maji ya kunywa na ali-pokunywa, aliendelea kusoma hukumu yake.

Wakati Hakimu Kabate anakaribia ukingoni kusoma hukumu yake, mshtakiwa Allawi alionekana akihangaika ndani ya kizimba cha mahakama, akivua kofia na kujifunika kwa kitambaa kichwani huku macho yake yakiwa mekundu mithili ya mtu anayelia.

Hakimu alisema kuwa baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi tisa na vielelezo 11 vya upande wa Jamhuri na utetezi wa washtakiwa, upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka mawili ya matumizi mabaya ya madaraka.

Kutokana na upande wa Jamhuri kuthibitisha mashtaka dhidi yao, washitakiwa wamepatikana na hatia kwa mashtaka yote mawili.

Pia alisema amesikiliza maelezo ya kupunguziwa adhabu, naye kama baba wa familia, ameguswa kwa mazingira ya baba kutokuwapo nyumbani, hivyo anawahukumu kifungo cha miezi sita

jela kila mmoja na rufani iko wazi kwa pande zote mbili.

Hakimu huyo pia alisema katika hukumu yake alizingatia kwamba washtakiwa hao waliongoza vyema chama hicho na hawakuwahi kuitisha migomo, hivyo katika kipindi cha uongozi wao, kuna mambo mazuri wamefanya.

“Kilichotokea ni kwamba hawa washtakiwa wameteleza kidogo kutokuwa makini katika vocha ya malipo. Kwa hiyo, wakikaa ndani miezi sita jela watajutia,” Hakimu Kabate alisema.

Kabla ya Kabate kutoa adhabu hiyo, Wakili wa Serikali, Imma Ntume, alidai mahakamani kwamba hawana rekodi za nyuma za washtakiwa kutenda makosa ya jinai, lakini akaomba adhabu kali kwa washtakiwa ili iwe fundisho kwa wao na viongozi wengine.

“Kutokana na nafasi za washtakiwa walizokuwa nazo, walikuwa wanapokea michango ya walimu kwa sababu waliwaamini. Mahakama itoe adhabu

kali ikiwamo kurudisha fedha walizotumia kwa manufaa yao binafsi,” Wakili Ntume alidai.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa Seif, Nesto Mkoba, aliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa sababu ni mgonjwa, anaishi na mama yake mwenye umri wa miaka 83 na pia ana mke na watoto wanne wanaomtegemea.

Mshtakiwa wa pili, Allawi, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia inayomtegemea, akiwamo mama yake mzazi mwenye umri wa miaka 90, mke na watoto sita na kwamba mtoto wa kwanza ni mwanafunzi wa chuo.

Baada ya hukumu, Wakili Mkoba alidai mahakamani kwamba wana nia ya kukata rufani Mahakama Kuu kupinga hukumu hiyo, hivyo aliomba mahakama iwapatie nakala ya hukumu na mwenendo wa kesi kwa ajili ya kukata rufani.

Washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Oktoba 3, 2018 na Novemba 6, 2018, katika ofisi za CWT

zilizoko Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wakiwa waajiriwa wa chama hicho, walitumia mam-laka yao vibaya kwa kujipatia Sh. 13,930,693 (Sh. milioni 13.93).

Katika shtaka la pili, siku na maeneo hayo, Seif na Allawi kwa kutumia madaraka yao vibaya na kwa manufaa yao wenyewe, wanadaiwa kuchepusha Sh. milioni 13.9 ambazo ni mali ya CWT.

Viongozi hao wanadaiwa kutumia fedha hizo kwa ajili ya safari ya kwenda Cape Verde kuangalia mechi ya mpira wa miguu.

NJE YA MAHAKAMA

Baada ya hukumu hiyo kusomwa, washtakiwa wakiwa chini ya Jeshi la Polisi, baadhi ya ndugu, jamaa na marafiki walionekana na kusikika wakiangua kilio mahakamani.

Pia, baadhi ya ndugu hao na wafanyakazi wenzao walionekana wamesimama kwa makundi wakisitika na wengine kupeana pole kwa kilichoajiri mahakamani.

HABARI KITAIFA**CHADEMA yaondoa kortini mapingamizi dhidi kina Mdee**

Na Grace Gurisha

MAHAKAMA Kuu Masjale Kuu Dar es Salaam leo inanza kusikiliza maombi yaliyowasilishwa na Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, na wenzake 18 baada ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuondoa mapingamizi matatu dhidi yao.

Vilevile, mahakama hiyo imetoa amri wabunge hao waendeleo kubakia katika nafasi zao hadi pale maombi ya kesi ya kuomba kibali cha kufungua kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Jaji Mustapha Ismail alitoa amri hiyo jana baada ya wajibu maombi wa kwanza kupitia mawakili wao, wakiongozwa na Peter Kibatata, kuomba kuondoa mapingamizi ya awali waliyoyaweka dhidi ya maombi hayo. Kibatata aliiambia mahakama kuwa mapingamizi hayo yalikuwa yameambatana na kiapo kinzani ambacho nacho wanaomba mahakama ikiondoe mahakamani ili maombi ya msingi yasikilizwe.

Alidai kuwa wameamua kuyaondoa mapingamizi hayo kutokana na kuzingatia kanuni kwamba maombi ya msingi yanatakiwa yasikilizwe ndani ya siku 14 tangu yafunguliwe, hivyo wakiendelea na mapingamizi hayo, yatasababisha kushindwa kumaliza shauri kwa wakati.

Pia alidai hawana pingamizi na amri za muda zinazotolewa, hivyo wanaichia mahakama ili waende kwenye hoja za msingi.

Baada ya Kibatata kudai hayo, mjibu maombi wa pili, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na mjibu maombi wa tatu (Tume ya Taifa ya Uchaguzi-NEC) hawakuwa na pingamizi juu ya ombi la Wakili Kibatata.

"Na sisi baada ya kusikiliza tunakubaliana na Kibatata kwa sababu maombi ya msingi yameletwa chini ya hati ya dharura na yanatakiwa yasikilizwe ndani ya siku 14 na pia hatuna pingamizi na amri za muda zinazotolewa," alidai Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola.


Wakili wa Mdee, Ipilinga Panya, alikubaliana na ombi la Kibatata, pia wakiiomba mahakama iyaondoe mapingamizi yao sita yaliyowasilishwa mahakamani hapo ili waende kwa muda. Jaji Ismail baada ya kusikiliza maombi hayo na kwa kuzingatia utendaji haki, alisema kwa sababu pande zote wamekubaliana kuondoa mapingamizi yao, mahakama inayaondoa na hayataendelea tena.

Pia aliamuru wabunge hao waendeleo kubakia katika nafasi zao hadi pale maombi ya msingi yatakaposikilizwa na kuamuliwa kutokana na kwamba hakuna upande uliopinga amri za muda.

Hata hivyo, Jaji aliiwaruhusu CHADEMA, NEC na AG kuwasilisha kiapo kinzani mahakamani hapo leo kabla ya saa nne asubuhi kabla ya kesi ya msingi kuanza kusikilizwa.

Juni 22 mwaka huu, mbele ya Jaji John Mgeta, mahakama hiyo iliondoa shauri kama hilo lililofunguliwa awali na wabunge hao baada ya kukubaliana na pingamizi la awali liliowasilishwa na mawakili wa CHADEMA.

Wabunge na wanachama hao wa zamani wa CHADEMA walivuliwa rasmi uanachama wa chama hicho usiku wa kuumkia Mei 12, 2022 baada ya Baraza Kuu la chama hicho kutupilia mbali rufani zao walizozikata wakipinga uamuzi wa Kamati Kuu iliyowavua uanachama.



Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa NALA, Benjamin Fernandes, akibadilishana mkataba wa ushirikiano mpya kati ya Selcom na NALA jijini Dar es Salaam juzi na Mkurugenzi Mkuu wa Selcom, Sameer Hirji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Saa sita za madaktari 31 kutenganisha pacha MNH

Na Romana Mallya

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) kesho inatarajia kufanya upasuaji mkubwa utakaochukua zaidi ya saa sita kutenganisha watoto pacha wawili wenye umri wa miezi tisa waliozaliwa wakiwa wameungana sehemu ya kifua na tumbo, huku umbo la ndani wakiunganina ini.

Daktari Bingwa Mshauri Mwelekezi wa Upasuaji wa Watoto, Petronila Ngiloi, alibainisha hayo jana hospitalini huko na kueleza kuwa upasuaji huo utahusisha madaktari 31.

Alisema kuwa kati yao, wataalamu wa ndani watakuwa 26 na wanaotoka nje watano wakiongozwa na Prof. Martin Corbally wa Bahrain ambao wamedhaminiwa na taasisi isiyo ya kiserikali ijulikanayo kama Operation Child Life ya Ireland.

Dk. Ngiloi alisema watoto hao (wote wa kike) kila mmoja ana ini lake na kufanyika kwa upasuaji huo kunaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu barani Afrika kuufanya baada ya Afrika ya Kusini na Misri.

Akizungumzia historia yao, alisema watoto hao walizaliwa Septemba 21 mwaka jana katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu kwa njia ya upasuaji wakiwa na kilo 4.9 wote kwa pamoja.

Alisema kuwa baada ya kuzaliwa, walipewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bugando) na Novemba 12 mwaka jana walipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili wakiwa na uzito wa kilo saba na sasa wana uzito wa kilo 13.3.

Alisema watoto hao ni wakazi wa Kijiji cha Mwabayande, Kata ya Mwigwa.

"Kufanyiwa kwa upasuaji huu kuna tokana na usimamizi mahiri wa uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili inayosimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji, Prof. Lawrence Museru, wa kuimarisha miundombinu stahiki ya kutolea huduma hizo ikiwamo vyumba vya upasuaji na ICU zenye vifaa vya kisasa vya kuhimili aina hii ya upasuaji pamoja na kusomesha wataalamu wa kutoa huduma hizo kwa kiwango cha ubobezi," alisifu.

Alisema upasuaji huo ni mkubwa, hivyo watoto hao wasingeweza kutenganishwa wakiwa na umri na uzito mdogo kwa sababu wanapokuwa wakubwa kuanzia miezi saba hadi 10, kunakuwa na usalama zaidi kwa kuwa wanaweza kuhimili hata dawa za usingizi na ganzi kulingana na aina ya upasuaji watakaofanyiwa.

Daktari huyo alisema kama wangepolekwa nje ya nchi, upasuaji huo ungeharimu karibu Sh. milioni 120, ziki-jumuisha gharama za usafiri wa mama, watoto wawili na msindikizaji mmoja.

Alisema kuna gharama za ziada za kufanya maandalizi ya watoto hao ikiwamo lishe na matibabu mengine ili kufikia kiwango cha kufanyiwa upasuaji wa kutenganishwa.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto, Zaitun Bokhary, alisema hospitali imefanya maandalizi yote stahiki yanayohitajika ikiwamo jopo la madaktari bingwa wa upasuaji watoto.

"Tumefanya maandalizi ya madaktari wa upasuaji viungo watoto, upasuaji ini, plastic surgery, wataalamu wa dawa za usingizi, wataalamu wa uangal-

izi maalum, wataalamu wa radiologia, wauguzi na wataalamu wa maabara.

"Wataalamu wa ndani watakuwa 26 na wanaotoka nje ni watano, wakiongozwa na Prof. Martin Corbally wa Bahrain. Wataalamu kutoka nje wamedhaminiwa na taasisi isiyo ya kiserikali ijulikanayo kama Operation Child Life ya Ireland." alifafanua.

Alisema kuwa baada ya upasuaji huo, watakuwa na kidonda kikubwa kutokana na kutenganishwa kifua na tumbo walipoungana.

Mtaalamu huyo alisema ili kukubaliana na hilo, Juni Mosi mwaka huu, waliwafanya upasuaji mdogo wa kuongeza ukubwa wa ngozi ili kutanua na kuongeza ngozi itakayosaidia kufunga kidonda mara baada ya upasuaji, hivyo kuwezesha kidonda kupona mapema.

"Baada ya upasuaji kama huu ni lazima kuwe na timu mbili ambazo kila timu itakuwa na majukumu yake, mara tu baada ya kutenganishwa kila timu itashughulika na mtoto mmoja ili kukamilisha upasuaji, watoto hawa watakaa ICU kwa siku mbili kisha kupelekwa wodi za kawaida," alisema.

Aliongeza kuwa upasuaji kama huo ni kwa mara ya tatu kufanyika nchini, wa kwanza ulifanyika mwaka 1994 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi tisa na wanaendelea vizuri.

"Upasuaji wa pili ulifanyika mwaka 2018 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi tisa na wanaendelea vizuri.

"Tunaishukuru Benki ya UBA kuwajengea makazi bora ambako wanaishi hadi sasa," alipongeza.

JMT: Sensa haina dini, ni ya watu wote

Na Jenifer Gilla

MWENYEKITI wa Kamati za Amani na Jumuiya za Maridhiano Tanzania (JMT), Shekhe Dk. Alhad Mussa, amesema Sensa ya Watu na Makazi haina dini na kuwaasa waamini kusimama pamoja kushiriki.

Aliyasema hayo jamaa jijini Dar es Salaam katika Kongamano la Kitaifa la Viongozi wa Dini kuhusu Sensa ya Watu na Makazi 2022, lililoandaliwa na JMT.

"Ninasema haya kwa sababu maalum, wapo watu ambao hawaoni sawa haya mahusiano yetu, kwamba kwa nini ninyi Waislam na Wakristo mnakaa pamoja. Tunakaa pamoja katika mambo ya msingi, ya kitaifa kama sensa, sensa haina dini, ni suala ambalo ni la watu wote," alisema.

Shekhe Mkuu huyo wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema kuwa kamati hizo msingi wake ni kudumisha amani na sio dini na ndiyo maana wanahamasisha watu kuhesabiwa bila kuangalia dini zao kwa kuwa vitabu vya

dini vinaonyesha kuwa binadamu wote ni ndugu.

"Kuna undugu wa ki-nchi, watu wakiwa wanaishi nchi moja, wao ni ndugu, lakini kuna undugu wa kibinadamu kwamba watu wote sisi tunatokana na Adam na Hawa sio? Na undugu huu umetajwa ndani ya Quran katika aya nyingi tu," alifafanua.

Mgeni rasmi katika kongamano hilo, Spika wa Bunge la Tanzania, Tulia Akson, ambaye pia ni mjumbe wa kamati hiyo, alisema sensa ya mwaka huu ni tofauti kwa sababu haiangalii hesabu za watu pekee bali nyanja zote za maendeleo na kufanikisha upatikanaji wa huduma muhimu za jamii ikiwamo ajira.

"Sensa hii inaangalia huduma zinazotolewa katika hayo maeoneo ambayo watu wamehesabiwa, kwa hiyo alivyotoa wito (Rais Samia) kwamba tuhakikishe sote tunashiriki na tushiriki kikamilifu, kwa maana ya sisi kuhesabiwa na kuhamasisha wengine wahesabiwe," alisema.

Pia aliitaka jamii kuitikia wito

wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha kuwa kila mmoja anahesabiwa bila kuwaacha nyuma wenye ulemavu kwa kuwa limekuwa kundi linalosahaulika.

"Ni muhimu sana wazazi, majirani tuhakikishe wale watoto ama watu wazima wenye ulemavu watu wote tuone ni jukumu letu kuhakikisha jamii zinawatoa hao watoto ili wahesabiwe, lakini hata watu wazima wenye ulemavu nao wahesabiwe," alisisitiza.

Aliwaomba viongozi wa dini kuhamasisha waumini wao katika maeneo mbalimbali ya nchi kuhusu kuhesabiwa kwa sababu jamii inawaamini na kusisitiza kuwa sensa haina uhusiano na dini, kodi wala siasa.

"Takwimu hizi zinazotafutwa ndugu Watanzania wenzangu hazina uhusiano na dini...lakini hazina uhusiano na kodi, mtu asiseme kuwa tunahesabiwa ili tulipe kodi, unahesabiwa ili kodi unayolipa ije ikuhudumie vizuri. Lakini haina uhusiano na siasa... wewe ni mwananchi wa Tanzania kwanza, halafu chama

kinakuja baadaye," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana, Jimbo la Dar es Salaam, Jackson Sosthenes, ambaye ni Katibu Mkuu wa JMT, alisema sensa ni agizo la Mungu kwa kuwa Biblia takatifu inaonyesha kuwa sensa ilikuwapo katika Taifa la Israel na ilifhamika kama ni usajiri wa watu wenye imani moja.

"Biblia inaonyesha kuna sensa mbili ambazo zilifanyika wakati wa Musa, lakini kuna sensa ilifanyika wakati wa Mfalme Daudi, sensa wakati wa Mfalme Selemani, wakati wa Nabii Nehemia na wakati wa Mfalme Agostino Warumi, kipindi cha kuzaliwa Yesu Kristo," alisema.

Kadhalika, alisema historia na maandiko inathibitisha wazi kuwa umuhimu wa sensa kwa taifa la Mungu ilikuwa ni umuhimu wa mambo mengi ya msingi ambayo mpaka sasa jamii inayahitaji ikiwamo kujua idadi ya watu kitaifa na nguvu kazi na rasilimali za watu wenye uwezo wa kufanya shughuli za uzalishaji na kulipa kodi.

WB yatoa bilioni 120/- kuboresha mahakama

Na Renatha Msungu, DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema katika mwaka wa fedha 2022/23, Benki ya Dunia imetoa mkopo wa masharti nafuu wa zaidi ya Sh. bilioni 210 ili kuboresha miundombinu ya mahakama nchini.

Prof. Juma aliyasema hayo jamaa alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama, lililofanyika jijini hapo.

Alisema mkopo huo unalenga kuimarisha miundombinu ya mahakama ili kufanya kazi katika mazingira mazuri.

"Serikali ya Tanzania hivi karibuni imepata mkopo wa gharama nafuu wa Dola za Marekani milioni 90 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 210 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya mahakama kwa mwaka ujao wa fedha," alisema.

Alisema Wizara ya Fedha na Mi-pango imekuwa ikitoa fedha kwa wakati katika miradi ya maendeleo inayoendelea huku Sh. bilioni 3.5 zikiokolewa.

Alisema fedha zilizoakolewa zimetumika katika ununuzi wa vitendea kazi vya mahakama ili kurahisisha utoaji haki kwa jamii.

Alisema wataendelea kusimamia vizuri fedha hizo na kudai kuwa mpango wa kuboresha miundombinu ni endelevu na kwamba umetajwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano.

Aliwataka watumishi wa mahakama kuwa wavumilivu wakati wanaendelea kufuatilia suala la upandishaji vyeo kwa watumishi wa Mahakama za Mwanzo.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema hivi sasa vitendo vya rushwa mahakamani vimepungua kutokana na utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya utafiti kwa taasisi za umma.

Alisema mwaka 2015 masuala ya malalamiko ya rushwa yalikuwa asilimia tisa, lakini hivi sasa imefikia asilimia tatu.

Aidha, alisema hadi kufikia Machi, 2022 walikuwa na watumishi 5,808 lakini watendaji wanahitajika ni 10,352 na upungufu wa watumishi ni 4,544.



Meneja Masoko na Mawasiliano wa Waendeshaji wa Bahati Nasibu wa Biko, Goodhope Heaven (kushoto), akiwa na furaha wakati akimkabidhi Sh. milioni 10 mshindi wao Gladness Gaiathan Lugenge mkazi wa Sinza, jijini Dar es Salaam, aliyeshinda kwenye droo kubwa iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. Kulia ni Meneja Uhusiano wa CRDB tawi la Premium, Ateeq Khan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mchakato wa bima ya afya kwa wote waiva

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummu Mwalimu, amesema wizara yake ipo katika hatua za mwisho za kuanza sheria itakayosimamia utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wote ili kuwapunguzia mzigo wa gharama kubwa za matibabu wananchi.

Alisema hayo jamaa jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukagua utoaji huduma na ujenzi wa jengo la wagonjwa walio chini ya uangalizi maalumu (ICU) katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alisema wizara ipo katika hatua za mwisho kuja na sheria

hiyo ambayo inatarajia kuipeleka bungeni mwezi Septemba ili kupitishwa na Bunge, kuanza kutumika ili kutoa ahuwani ya gharama kubwa za matibabu kwa wananchi.

"Wizara ipo katika hatua za mwisho kuja na sheria itakayosimamia utoaji wa huduma za bima ya afya kwa watu wote na kuondokana na bima ya afya ya jamii CHF, ambayo haitumiki katika baadhi ya maeoneo.

"Bima hii kwa wote tunataka iwe kama ile ambayo anapata hivi sasa mtumishi wa umma hii ya sasa ni sawa na kuwadanganya watu hasa katika vipimo vikubwa kama vya CT SCAN ambavyo

gharama zake juu mtu wa CHF hawezi kuzipata," alisema Mwalimu.

Alisema pamoja na serikali kuboresha miundombinu ya afya kwa kujenga majengo na kuweka vifaa tiba, lakini lengo kuu ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za matibabu za uhakika na bora.

"Tunataka kila Mtanzania kumudu gharama za matibabu kupitia mpango huu wa bima ya afya kwa wote siwezi kutaja kiwango cha gharama zitakavyokuwa, lakini Watanzania watuamini kuwa tunakwenda kuweka kiwango ambacho hata mtu wa chini ataweza kumudu kuanzia ngazi ya zahanati hadi ya rufani kama

vile Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisisitiza Mwalimu.

Aidha, alisema anapanga kukutana na wamiliki na wakuu wa shule zote za sekondari nchini ili kuona ni jinsi gani wanafunzi wote wanakuwa na bima za afya za NHIF.

"Lazima watoto wetu wa shule za sekondari kila mmoja awe na kadi ya NHIF ambayo wala sio gharama sana kwani mtoto mmoja ni Sh. 50,400, lazima wazazi waone umuhimu wa kuwakatia bima watoto wao katika vyuo hivi sasa ni lazima, lakini na huku lazima tukae tuweke makubaliano," alisema.

Aliuagiza uongozi wa hospitali hiyo kuhakikisha malalamiko am-

bayo yamekuwa yakitolewa na wananchi yanakwisha hasa muda ambao mtu anautumia kupata huduma usizidi saa tatu.

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Ibenzi Ernest, aliishukuru serikali ya awamu sita kwa kuwapatia fedha kiasi cha Shilingi bilioni nne kutoka fedha za mapambano ya UVIKO-19, ambazo wamezitumia kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo na ujenzi wa wodi ya ICU.

Hata hivyo, alisema hospitali hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa watumishi, msongamano wa wagonjwa na ufnyu wa wodi ya wazazi.

HABARI KITAIFA

TMDA yanasa dawa feki za kuongeza nguvu za kiume

Na Mary Geoffrey

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Mashariki imekamata vifaa tiba na dawa ambazo hazijasajiliwa zenye thamani ya Sh. milioni 294.4, zikiwamo za kuongeza nguvu za kiume.

Bidhaa hizo zimekamata kutokana na ukaguzi maalum uliofanyika Mtaa wa Kitumbini, Kata ya Mchafukoge, katikakati ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza eneo la tukio, Meneja wa Kanda wa TMDA, Adonis Bitegeko alisema:

“Timu ya TMDA Kanda ya Mashariki imefanya ukaguzi maalum katika ghala bubu kufuatia taarifa za kiintelijensia zilizofuatiliwa kwa muda mrefu.

“Katika ukaguzi tuliofanya, tumebaini ghala hili linalomilikiwa na Mtanzania mwenye asili ya India, Ramaiya Rijendra, limehifadhi dawa mbalimbali za binadamu ambazo hazijasajiliwa, kwa hiyo ubora, usalama na ufanisi wake haujulikani.”

Alitaja hatua zilizochukuliwa ni kuziondoa dawa hizo baada ya kuziorodhesha.

Aliongeza kuwa hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kuwatoza faini isi-yopungua Sh. milioni 85 na kuzitekeza kwa gharama zao.

Meneja huyo aliwasilhi wanaoendelea kufanya biashara hizo haramu kuacha mara moja, vinginevyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aliendelea kuonya pia wataalamu wa dawa wanaojihusisha na biashara hizo haramu kuwa hawatosita kuwafutia leseni zao za kitaaluma.

Alizitaja baadhi za dawa hizo ni pamoja na za shinikizo

la damu, za kuongeza nguvu za kiume, kutoa ujauzito na zingine nyingi.

“Rai yetu ni kwamba wale wote wanaofanya biashara haramu, adhabu ni kali na hatutumwacha mtu,” meneja huyo alionya.

Alibainisha kuwa ukaguzi huo ulianza Jumatatu jioni na kufanyika usiku kucha hadi ulipokamilika asubuhi ya juzi.

Mtuhumiwa aliyekutwa na dawa hizo, alipohojiwa alikiri kuendesha ghala hilo pasipo na kibali, jambo ambalo ni kinyume cha sheria na taratibu za nchi.

RC aagiza kukamatwa waliokula fedha mbichi

Na Happy Severine, BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ameliagiza Jeshi la Polisi kuwamakata watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani humo wanaodaiwa ‘kutafuna’ Sh. milioni 52 za makusanyo ya ushuru zilizokusanywa kwa kutumia mashine za kielektroniki.

Kafulila alitoa agizo hilo jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani humo kilichojadili hoja za Mkaguzi na Mdhidhi wa Hesabu za Serikali (CAG) kilichofanyika mjini Bariadi.

“Hao watu walikula hela mbichi?” Alihoji RC Kafulila akiamaanisha fedha za makusanyo ya ushuru zilizotumika kabla ya kupelekwa benki.

Alisema majina ya watumishi wanaotuhumiwa yakabidhiwe kwa Kamanda wa Polisi mkoani Simiyu, Blasius Chatanda, kwa hatua zaidi za kisheria.

Aliongeza kuwa fedha hizo ni za serikali, hivyo mtu yeyote anayezitafuna kinyume cha sheria, lazima akabiliwe na shinikizo la sheria.

“RPC kamata, tupa ndani waka siku mbili, ili watoe maelezo vizuri kwa sababu hili ni kosa kubwa. RPC upo?” Alihoji RC Kafulila huku RPC Chatanda akiitikia ‘nipo mkuu, nina hamu nao’, kauli iliyoibua kicheko kwenye kikao hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Adrian Jovin Jungu, alisema tayari watu waliokula fedha Sh. milioni 81 wameshaanza kuzirejesha.

“Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, majina (ya wanaotuhumiwa kula fedha) tunayo na tumeshapeleka ofisi ya TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kwa ajili ya hatua mbalimbali.

“Na tunashukuru sana kwa kufanya kazi kubwa, baadhi yao wamesharejesha kati ya Sh. milioni 81 ambazo walikuwa wamezila, Sh. milioni 20 zimerudi,” alisema Jungu na kuongeza:

“Majina wanayo TAKUKURU, wanaendelea na utaratibu kwa hatua dhidi yao.”

Katika hatua nyingine, Kafulila kupitia kikao hicho, alionya kuwa kuanzia Julai 27 mwaka huu, mizani yote ya kupimia pamba itakayokamatwa ikiwa imechezewa ili kumwibia mkulima, lazima mhusika akamatwe na kulala mahabusu walau kwa saa 48.

Alisema mbali na kulala huko, mzani utakaonaswa umechezewa, utanyang’anywa hadi msimu wa ununuzi pamba utakapohitishwa.

“Kwenye kilimo kuna nguvu na jasho kubwa huwatoka wakulima, halafu leo mtu aje achezee jasho hilo. Haiwezekani mtu achezee mzani kumwibia mkulima, tumkamate arekebishiwe mzani aachwe nao, kesho atachokona tena.

“Tukikukamata faini Sh. milioni mbili za kisheria na mzani tunaushikilia hadi mwisho wa msimu wa mavuno,” Kafulila alionya.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation, Dk. Hellen Senkoro (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuwapo kwa mdahalo wa kumbukizi ya maisha ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa, utakaofanyika Kisiwani Zanzibar Julai. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Nape: Wanahabari bado wanakabiliwa na matatizo

Na Gwamaka Alipipi

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema sekta ya habari nchini bado inakabiliwa na matatizo lukuki ambayo yanapaswa kutatuliwa kwa ushirikiano kati ya wadau husika na serikali.

Ameyataja matatizo hayo yanajumuisha taaluma hiyo kutotambulika kuwa na hadhi kama ilivyo kwa taaluma zingine, ujira mdogo kwa wanahabari, ucheleweshaji wa stahiki pamoja na kutoweka kwa uandishi wa habari za uchunguzi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kongamano la wahitimu wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC) katika mwendelezo wa sherehe za miaka 60 tangu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwaka

1961.

Kongamano hilo liliwakutanisha viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi binafsi walio-wahi kusoma katika shule hiyo.

Nape alisema taaluma ya habari imekuwa haipewi hadhi kama zilivyo taaluma zingine, akitolea mfano pindi mwandishi wa habari anapokosea kuandika habari, adhabu itakayotolewa ni kukifungia chombo husika badala ya adhabu kwa mhusika.

Nape alisema: “Mbona taaluma zingine kama udaktari, daktari akikosea haifungwi hospitali? Sasa tunahitahi kurekebisha vitu kama hivyo, tunataka taaluma ya habari iwe na hadhi kama zilivyo zingine, tunataka iheshimike.”

Alisema wanahabari wengi wamekuwa hawapewi mikataba ya ajira, kwamba wengi wao wanafanya kazi katika mazingira magumu huku wakiishia kulipwa ujira mdogo.

“Siku hizi hakuna uandishi wa habari za uchunguzi, jamii inaitupia lawana serikali, serikali inaitupia lawana vyombo vya habari na vyombo vya habari inavitupia lawana serikali, yaani kila mtu anamnyooshea kidole mwenzake. Tunapaswa tutoke huko,” Nape alishauri.

Kuhusu kongamano hiyo, Waziri Nape alitaka uongozi wa SJMC kujenga utaratibu wa kukutana na wahitimu wa miaka ya zamani kuzungumza nao na kupata tathmini ya hali ya maisha mtaani kwa kuweka mizania ya kujua kama elimu waliyopata inawasaidia katika maisha.

Alisema: “Ninatamani kuona makongamano kama haya yakiendelea kwa sababu yatatusaidia kujua ‘demands’ (mahitaji) zilizoko mtaani. Tunapaswa kuhakikisha tunachozalisha kinakwenda kutoka mtaani.”

Nape aliomba SJMC kusaidia kutoa mawazo katika mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Huduma ya Habari, ili iwe na tija katika tasnia ya habari nchini.

Amidi wa SJMC, Dk. Mona Mwakalinga, alitaja kero mbalimbali zinazoikabili shule hiyo, ikiwamo Kituo cha Televisheni cha Mlimani kutopatikana katika ving’amuzi, wafanyakazi na wanafunzi kupata fursa za elimu kimataifa.

Dk. Mwakalinga alisema: “Televisheni na Radio Mlimani hazipatikani katika ving’amuzi kama zilivyo chaneli zingine za nyumbani, tunaomba msaada wako katika suala hili kwani itasaidia kukitangaza chuo na Taifa.”

Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema UDSM tangu kuanzishwa kwake, imetoa viongozi wengi mashuhuri ndani na nje ya nchi.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

Matapeli wa kimtandao wadhibitwe ni kero

JUHUDI zinazofanywa na Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watu wanaojihusisha na uhalifu wa kimtandao, zinatoa matumaini kutokana na uhalifu huo kuongezeka siku hadi siku.

Wahalifu wanaotumia mtandao kuwalaghai na kuwaibia wananchi hutumia mbinu mbalimbali zinazowashawishi wananchi kuingia kwenye mtego wao.

Mbinu kubwa wanayoitumia na kuwapigia wateja wa simu wa kampuni mbalimbali za mitandao hiyo na kuwalaghai watume pesa ili waongezewe salio au kwa kuwadanganya jambo ambalo mteja atashawishika kuwaamini na kuwatumia pesa.

Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), katika kudhibiti hali hiyo ilizigiza kampuni za simu nchini kusajili laini zote kwa kutumia Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na alama za vidole, lakini cha kushangaza utapeli huo unaendelea na watu wengi wanalizwa kwa kuibiwa pesa zao bila kukamatwa.

Kuna ujumbe ulizoeleka kutumwa na matapeli hao kwenye simu za watu ukisomeka 'hiyo hela tuma kwa namba hii' ambao kwa sasa hauonekani sana baada ya wajanja hao kubaini kuwa watu wameshawang'amua.

Kuna vijana ambao hupita mitaani kwa kuwatangazia wananchi kuwa wanasajili laini za simu, ambao hudai kutumiwa na kampuni za simu, lakini haieleweki kama usajili huo unazingatia matakwa ya TCRA.

Pengine usajili huo unaweza kuwa moja ya chanzo cha kuwapo kwa matapeli hao ambao wanaweza kusajili laini zaidi ya moja na kuzifanyia utapeli na kisha kuzitupa.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, wahalifu zaidi ya 20 wamekamatwa jijini humo kwa kufanya uhalifu kwa njia ya mtandao.

Jeshi hilo linasema wahalifu hao hutumia mbinu ya kutuma ujumbe mbalimbali kupitia namba tofauti za simu wakionyesha nia ya kutaka kuwasaidia, kisha huwaibia.


Wahalifu hao walikutwa na vifaa mbalimbali wanavyovitumia kufanya uhalifu huo vikiwamo kompyuta mpakato, kompyuta za mezani, simu za aina tofauti, modemu za mitandao yote na kadi za simu za mitandao mbalimbali zaidi ya 50.

Jeshi hilo lilibaini pia mojawapo katika ujumbe wanaotumia wahalifu hao kuwaibia wananchi ni kuwadanganya wazazi kuwa watoto wao shuleni wamepata matatizo, au kuumwa sana na kutaka watume hela ili wawapeleke hospitali na wazazi wakituma wanakuwa wameibiwa.

Uhalifu mwingine ni mtu anapoibiwa simu na mwizi kutuma ujumbe kwa ndugu au marafiki wa aliyeibiwa simu awatumie pesa akidai amepatwa na tatizo kubwa. Mwizi huyo huomba kiasi kikubwa cha pesa na kama mtu hayuko makini anaweza kutuma akiamini kweli ndugu yake yuko kwenye matatizo.

Wengine hutumia mitandao ya simu kufanya mambo yasiyofaa kwenye jamii kwa kusambaza picha chafu kwa lengo la kumchafua mtu au kufanya biashara ya ukahaba kupitia njia hiyo ya mtandao.

Kazi inayofanywa na Jeshi la Polisi kuwakamata wahalifu hao itasaidia kupunguza vitendo hivyo ambavyo vimekuwa kero kwa jamii na kuharibu nia nzuri ya kuwapo kwa mitandao ya simu kurahisisha kazi mbalimbali ambazo siku za nyuma ilimbidi mtu aende moja kwa moja kupata huduma kama ya pesa au kulipia kitu.



Na Adam Fungamwango

Muongwana Lazima Nilonge

Kwa hili tunashuhudia serikali inavyopunguza msongo mawazo

WATAALAMU wa lugha ya Kiswahili, wanautaja msongo wa mawazo ni mfadhaiko wa akili anaupata mtu, kutokana na shida, tabu, dhiki au changamoto zinazomkabili katika maisha ya kila siku, hasa pale anaposhindwa namna ya kukabiliana nalo.

Wengine wanasema ni mawazo au hisia ya kutoweza kukabiliana na mahitaji yatoakanayo na kazi, uhusiano, shinikizo la kifedha na hali zingine kimaisha.

Mtu au binadamu akifikia hali hiyo, inatajwa kuwa hatari sana, kwani anaweza kufanya lolote kama kujidhuru au kumdhuru mwingine, hata kama hahusiki na mkasa wake.

Bungeni Dodoma, ilitangazwa serikali imekubali kupunguza tozo za miama ya simu na ving'amuzi, baada ya kufanyika majadiliano na Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Katika punguzo hilo, tozo ya ving'amuzi zimeshuka kutoka Sh.3, 000 hadi viwango kati ya Sh.500 na 2,000, tozo za miama ya simu nazo zikishuka kutoka Sh. 10,000 hadi Sh.4, 000.

Ni uamuzi, unaobeba suala la kuweka kando sharti la lazima kwa kila Mtanzania mwenye umri miaka 18, akinunua au kuuza bidhaa ni lazima awe na namba ya mlipa kodi (TIN).

Tuna ushuhuda siku kadhaa, serikali ikisikiliza sana maoni ya wananchi wake, hivi karibuni ilitoa Sh. Bilioni 100 kwa ajili ya ruzuku, kupunguza bei ya mafuta nchini.

Pia, Waziri wa Fedha na Mi-pango Dk. Mwigulu Nchemba, alipendekeza kufutwa ada kwa

wanafunzi wa kidato cha sita, ikiendeleza kuwapunguza wananchi gharama za maisha.

Naamini, bado serikali inaendelea na mipango mingine kuhakikisha mzigo haumuelemei mwananchi kwenye nyanja mbalimbali, ili kumboreshea maisha.

Niipongeze serikali kwa kuendelea kugusa sehemu zinazoonekana mwananchi anaumuia, hata kumuepushia msongo wa mawazo.

Ni hivi karibuni, kumekuwapo matukio mengi ya watu kujeruhiana au kuuana, hasa wanandoa, wapenzi, familia moja, mtu na baba yake au mtu na mama yake. Sababu nyingi zinatajwa, mojawapo ni msongo wa mawazo unaotokana na ugumu wa maisha.

Gharama za vitu mbalimbali na ugumu wa maisha zimekuwa zikisababisha hata matukio tunayoyaona na kuyashangaa, tukijiuliza "kwanini yameibuka kwa kasi hivi karibuni?"

Ni kweli, hata zamani wanandoa wamegombana, pia kuwapo migogoro kwenye familia, lakini hakukuwapo sana ushuhuda wa mengi ya kikatili kama ya sasa, ingawaje kidunia, hakuna kinachofanyika sasa ambacho ni kigeni duniani.

Itikadi, sera na siasa ya Ujamaa, kila kitu kumilikiwa na umma, huku wananchi wakipata bure mahitaji yao kama elimu, afya, maji na mengine yanayofanana na hayo.

Ni hatua iliyowanyima msongo mkubwa wa mawazo kiasi cha kuchanganyikiwa na kufanya maamuzi ya ajabu anapoudhiwa, japo kidogo.

Pia, hakukuwapo mahitaji mengi kama sasa, ikizingatiwa,

sasa kuna maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mtu alitafuta pesa ya chakula, nguo, nauli na mahitaji mwingine machache. Dunia nayo imebadilika na haiwezekani kuishi kama ilivyokuwa zamani. Kama nchi nyingine zilivyobadilika, Tanzania haikuachwa nyuma kwa mabadiliko ya sera na maendeleo ya teknolojia.

Kwa maana hiyo, mtu anaamka, anatakiwa pesa ya chakula, nauli za watoto shuleni, ada, bili ya umeme, maji, pesa ya kupeleka watoto hospitali na madeni juu.

Kutokana na maendeleo ya teknolojia hasa ya simu za mkononi, anatakiwa kuwa na salio lake wakati mwingine na mkewe, 'bando' kwenye simu, ili dunia iwe kiganjani.

Pia, mtu anatakiwa kulipia ving'amuzi ili watoto waangalie katuni, familia iangalie filamu na tamthilia, yeye mwenyewe aangalie soka.

Ukichanganya vitu hivyo, kuna wakati vinamtoa jasho au kumshinda kutokana na tozo za kodi na ushuru kuwa juu, hivyo kumsababishia msongo wa mawazo kutokana na kushindwa kuzimuda.

Mtu kama huyu akiudhika, au kuudhiwa na mwenzake, hata akichanganya na ugumu wa maisha, anaweza kufanya chochote kile. Sababu kuu ni uhalisia ulioelezewa.

Nirudie tena kusema, serikali imefanya hivi kwa mapenzi na wananchi wake, pia itakuwa kwa kiasi kikubwa inawapunguza wananchi wake msongo wa mawazo, kwani inawatua mzigo, maisha walau yawe na sura ya amani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

Mhariri Mtendaji: Beatrice Bandawe

Meneja Usambazaji na Masoko: Emmanuel Lyimo, 0716 500500

Mapokezi: 0745 700710

Matangazo: 0782 253676

Baruapepe: advertise@guardian.co.tz

Website: www.ipppmedia.com

www.epaper.ipppmedia.com

PUBLIC NOTICE

The Registrar of the Board under the powers conferred to him/her under section 10 (3) and regulation 4 (4) of the Private Health Laboratories Act, 1997 (No. 10 of 1997) is hereby giving Notice to the General Public, that the following is the list of Private Health Laboratories registered by the Board as at **1st July 2021 to 30th June 2022**

A: REGISTERED AUTONOMOUS PRIVATE HEALTH LABORATORIES

REGION	S/N REGION	NAME OF THE LABORATORY	HEALTH LAB. GROUP	REGISTRATION NO.	APPROVED PERSON (LAB. MANAGER)
ARUSHA	1	Nzunduka Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/001	Mary Mollel
	2	Highway Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/002	Fildorin Abdul Msami
	3	Curare Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/003	Estomih E. Ngira
	4	Bituri Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/005	Marco E. Mayo
	5	Tahfifu Modern	C	PHL-C/ARU/AUT/007	Fredrick E. Kiula
	6	Sekei Laboratory Services	C	PHL-C/ARU/AUT/009	Evans J. Nanyaro
	7	Black Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/010	Benedict G. Maembe
	8	New Kaloleni H. Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/011	Martha Mushi
	9	Dream Molecular Laboratory	B2	PHL-B2/ARU/AUT/012	Michael D. Ngonyani
	10	Agape Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/014	Innocent R. Kimaro
	11	Charity Modern Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/017	Fredrick Kiula
	12	Fame Medical Laboratory	B2	PHL-B2/ARU/AUT/019	Anton S. Marley
	13	Arusha Centre Diagnostic Lab.	C	PHL-C/ARU/AUT/020	Estomih E. Ngira
	14	Tumaini Jema Med. Lab.	C	PHL-C/ARU/AUT/023	Habiye Laway Yamay
	15	Arusha Junior Human Lab.	C	PHL-C/ARU/AUT/024	Phanuel G. Anney
	16	Amani GF Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/027	George J. Mrema
	17	Jibabha Health Lab. Services	C	PHL-C/ARU/AUT/033	Joseph Gerson Mgas
	18	Safe Focus Laboratory	B2	PHL-B2/ARU/AUT/034	Eva E. Mbwilo
	19	Modern Clinical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/035	Herman Julius
	20	Megacare Laboatory	B2	PHL-B2/ARU/AUT/037	Petero L. Massawe
	21	MICO Palloth Lab. Services	C	PHL-C/ARU/AUT/038	Habiye Laway Yamay
	22	Neema Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/039	Martha Mushi
	23	Meserani Laboartory	C	PHL-C/ARU/AUT/040	Anastazia N. Qayamo
	24	Agape Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/041	Anastazia N. Qayamo
	25	Usanda Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/044	Joseph Gerson Mgas
	26	Shamsi Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/046	Lilian E. Mkony
	27	Focus Human Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/049	Emmanue Munna
	28	Elgibo Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/051	Loema P. Soya
	29	Sakim Medical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/052	Ivo Mbowe
	30	True Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/053	Imani S. Nkolela
	31	Safari Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/054	Rose G. Bogohe
	32	Prince Med. Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/056	Rehema Vegula
	33	Respect Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/059	James Mziray
	34	Kuhenga Annex Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/060	Lucas J. Jamberi
	35	Egaden Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/061	Justa Cassius
	36	Victory Lab. Health Service	C	PHL-C/ARU/AUT/062	Joseph Gerson Mgas
	37	Avita Care Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/064	Mwanaidi P. Kudra
	38	Baraa Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/066	Paskalina L. Sanga
	39	Kisongo Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/067	Thomas Mjungu
	40	FM Healthcare Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/068	Frank F. Maleo
	41	Qube Diagnostic Lab. Services	C	PHL-C/ARU/AUT/069	Eugenia A. Kibunku
	42	Tras Medical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/070	Ombeni Mwanga
	43	Megacare Laboatory	B2	PHL-B2/ARU/AUT/071	Paterno L. Massawe
	44	Majengo Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/072	Jumanne S. Lomay
	45	FIL Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/073	Philipo M. Peter
	46	ORBIT Polyclinic & Diagnostic	C	PHL-C/ARU/AUT/074	Revocatus G. Chuwa
	47	Ashengai Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/076	Kasembo S. Kulwa
	48	Kisau Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/077	Evan J. Nanyaro
	49	HI-TEK BIOLAB	C	PHL-C/ARU/AUT/078	Praygod C. Kitiiri
	50	USA Medical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/079	Ivo E. Mbowe
	51	Sunlight Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/080	Regnald M. Ngoli
	52	Oiasiti Smart Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/081	Nehemia J. Mshote
	53	R&D Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/082	Biesha W. Kinunda
	54	St. Peter Diagnostic Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/083	Augustino J. Lukindo
	55	Life Line Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/084	Fadhili J. Ngowi
	56	Bene Modern Medical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/085	Salum Nyerere
	57	Edeni Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/086	Justar C. Mawangala
	58	Dr. Pashuna Diagnostic Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/087	Neema B. Honest
	59	Murick Medical Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/088	Elihuruma F. Ngowi
	60	Criti Care Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/089	Evince E. Matee
	61	Mulla Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/090	Mary A. Mollel
	62	Weledi Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/091	Lucas F. Kibajaw
	63	Wanjira Human H. Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/092	Frank Z. Lukumay
	64	Madina Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/093	Ernest J. Kazungu
	65	Alishina Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/094	Emmanuel M. Charles
	66	Nazareth Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/095	Cosmas G. Muray
	67	Kirayi Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/096	Emmanuel O. Sumari
	68	Dareda Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/097	Lucas J. Jamberi
	69	Solidodi Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/098	Severa M. Massawe
	70	MF Care Health Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/099	Innocent Rogasian
	71	New Life Scope Laboratory	C	PHL-C/ARU/AUT/100	Alex J. Andreson

REGION	S/N REGION	NAME OF THE LABORATORY	HEALTH LAB. GROUP	REGISTRATION NO.	APPROVED PERSONAL (LAB. MANAGER)
DSM ILALA	1	Amref Laboratory	A Single Purpose	PHL-A Single Purpose/DSM-ILA/AUT/002	Okumu A. Were
	2	ECLA Health Laboratory	C	PHL-C/DSM-ILA/AUT/004	Bakari Chambuso
	92	Mtani Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/088	Neema J. Maeda
	93	Namweta Njepeni Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/089	Naftali Amani
	94	Afya Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/090	Jeronimo O. Kasebula
	95	ST. Joseph Collage of Engineering Disp.	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/091	Nasibu Said
	96	Kibangu Hospital	B2	PHL-B2/DSM-UBG/ATT/092	Andrea S. Chanai
	97	Prime Care Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/094	Fahim A. Ibrahim
	98	K-G Afya Care Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/095	Didas M. Kamuzora
	99	Joan Msakuzi Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/096	Rachel W. Ndallu
	100	Medway Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/098	Rehema M. Dedano
	101	MICO Kimara Tanesco Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/099	Pili B. Masala
	102	Jambo Specialized Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/100	Filbert Jiskaka
	103	St. Philipo Dispensary	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/101	Philipo Mcharo
	104	Zomola Specialized Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/102	Editha M. Mayalla
	105	KAM Musika Hospital	B2	PHL-B2/DSM-UBG/ATT/103	Siangicha G. Mtui
	106	Kairuki Polyclinic	B2	PHL-B2/DSM-UBG/ATT/104	Maliki S. Maliki
	107	Kilungule Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/105	Neema A. Mshana
	108	Salba Medical Care Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/106	Samwel M. Mhina
	109	MICO Charitable Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/107	Elia M. Gundi
	110	Sokeny Polyclinic	C	PHL-C/DSM-UBG/ATT/108	Michael L. Lulambo
	111	Jilyendyage Dispensary	C	PHL-C/DSM-UB	


MATANGAZO MCHANGANYIKO

FORM 58
IN THE DISTRICT COURT OF TEMKE
AT ONE STOP CENTRE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO
541 OF 2022
In the Matter of the Estate of the Late
MASINDIKO RINGIA SHAO
and
In the Matter of Application for Letters of
Administration by
PAULINA JOSEPH SHAO
GENERAL CITATION
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12 day of 8, 2022.

Dated at DAR ES SALAAM this 28 day of 6, 2022.



Registrar/Senior Resident Magistrate

KUPOTEA
KWA VYETI



JONES SOSTHENES MUTA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0800/0134/2012** na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0800/0637/2015** vyote vilitolewa na Baraza La Mithani la Taifa kupitia **LOYOLA HIGH SCHOOL**. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: DAR/KIM/RB/237833/2022

MM AUCTIONEERS & DEBT COLLECTORS CO.LTD
TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu wa benki ya KCB tutauza kwa mnada wa hadhara mali/dhama ya mdaiwa wa Benki, kama ilivyoorodheshwa hapo chini, mnada utafanyika kama ifuatavyo:-

- **KIWANJA NA. 574, KILICHOPO MINJINGU WILAYA YA BABATI, C.T NA 28162, MALI YA PHILIP SANG'KA MARMO AMBAYE NI MDHAMINI WA VILLAGE PEOPLE ENTERPRISES, MNADA UTAFANYIKA TAREHE 10/07/2022 KUANZIA SAA 4.00 ASUBUHI NA KUENDELEA**

MASHARTI YA MNADA
 Mnunzi anatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na salio la asilimia 75% anatakiwa kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya mnada.


Mnunuzi akishindwa kulipa salio la asilimia 75% ndani ya siku kumi na nne (14) atakuwa amepoteza haki zake zote pamoja na asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.

Nyumba inaweza kukaguliwa kuanzia tarehe ya tangazo hili mpaka siku ya mnada.

Mnunuzi anatakiwa kusimamia mwenyewe zoezi la kubadili hati ya kumiliki/mali aliyonunua na kulipa kodi zote stahiki. Nyumba/mali itauzwa mahali na kama ilivyo

Wote mnakaribishwa
MM AUCTIONEERS & DEBT COLLECTORS CO. LTD.
S.L.P 20306, DAR ES SALAAM
SIMU: 0755404801/0715401801

KUPOTEA
KWA CHETI



FESTO N. MALEBETO anatangaza kupotelewa na cheti cha **ORDINARY DIPLOMA IN PRIMARY EDUCATION** chenye No. **NS1196/0049/2007** kilichotolewa na **CAPITAL TEACHERS' COLLEGE** mwaka **2018**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/256157/2022.**

KUPOTEA KWA
KADI YA GARI


OBOTE NDYABALILA
KALIMAGI ANATANGAZA
KUPOTELEWA NA KADI YA
GARI AINA YA TOYOTA NOAH
YENYE NAMBA ZA USAJILI
T 276 DHL YENYE CHASSIS
NO. SR400127356 NA ENGINE
NO. 355057150
KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA
ATOE TAARIFA KITUO
CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
KAH /RB/ 718/2022

SAMBA SERVICE COMPANY LIMITED
M/S MICHKA AGRO BUSINESS
LTD.....MWOMBAJI
DHIDI YA
ELIZEUS KANYANGONGA NA WENZAKE
13WAJIBU MAOMBI

Kwa idhini niliyopewa na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya Bukoba, siku ya Ijumaa tarehe 01/07/2022 Kampuni ya Samba Service Company Limited itauza kwa mnada wa hadhara ng'ombe mali ya wajibu maombi.

Mnada huo utaanza majira ya saa 4:00 asubuhi maeneo ya Akamea Kihanga Mnadani. Mnunuzi atalazimika kulipa kiasi chote cha fedha kilichofikiwa.

Wako,




AZATH JUMA SIMBA
DALALI WA MAHAKAMA (M) KAGERA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA
Kituo cha MJINI TANGA Mkoa wa TANGA
Shauri la Madai Na. 169/2018
Jina la Mdai: DARUSI NG'ANZI ULENGE
Jina la Mdaiwa: ALLY RAMADHANI KONDOO
KUITWA SHAURINI
Kwa: ALLY RAMADHANI KONDOO
C/O MW/KITI MWAKIDIKI
Kwa kuwa Mdai/Wadai/Ameleta/Wameleta madai
yake/yao kwamba
MADAI YA URITHI

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 6 Mwezi 09 Mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa umepokea wito kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila weve kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 23/6/2022.



KUPOTEA
KWA VYETI



ROSEMARY MOSES SENDU anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1549-0047** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ENGUTOTO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2012** na cheti cha chuo cha ualimu chenye usajili namba **E0520-0082** kilichotolewa na **SINGACHINI TEACHER TRAINING COLLEGE 2015. ARU/ARU/RB/417330/2019**

Uza, Chenye Thamani

Kubwa Kwa

Kutangaza Nasi Kwa

Bei Poa Tupigie

0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

KWA HABARI MOTOMOTO
USIKOSE GAZETI
LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

Mulamula aanika walichoteta Kigali

Na Halfani Chusi

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, ametaja mambo sita ambayo alishiriki na kuyajadili katika ziara ya siku saba aliyofanya Rwanda hivi karibuni.

Balozi Mulamula alihudhuria mkutano wa 26 wa wakuu wa nchi na Jumuiya ya Madola uliofanyika jijini Kigali kuanzia Juni 19 hadi 15 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam



jana, Mulamula alisema mkutano huo pia ulihudhuriwa na Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi wa serikali 27 kutoka katika nchi 54, ulijikita katika maeneo kadhaa ikiwamo utawala bora, utawala wa sheria na haki za binadamu.

Mengine ni yanayohusu vijana, afya, teknolojia na uvumbuzi, uendelevu kwenye masuala ya biashara kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi

na utunzaji wa mazingira.

“Ukiangalia mambo haya yote yanaendana na sera ya Rais Samia, kitu ambacho kilitusukuma kushiriki kwa moyo mmoja katika mkutano huo, lakini kulikuwa na mambo mengi tuliyoyajadili katika mkutano huo ambao ulitanguliwa na mikutano kadhaa iliyohusu majukwaa ya Jumuiya ya Madola na mawaziri wa mambo ya nje.

Balozi Mulamula alisema: “Katika jukwaa la biashara, ujumbe wa Tanzania ulijadili fursa za biashara na uwekezaji kwenye Jumuiya ya Madola na Bara la Afrika na matatizo mbalimbali

yanayoikabili sekta hiyo ikiwamo ugonjwa wa corona.”

Alisema pia kulijadiliwa mgogoro uliopo kati ya Ukraine na Urusi, ujumbe huo ukiwasilishwa na Dk. Twalib Abdallah, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Sekta ya Viwanda na Biashara.

Balozi Mulamula alisema katika jukwaa la wanawake, Tanzania iliwakilishwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto, Abeida Rashid, kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema jukwaa hilo lilijadili usawa wa kijinsia na jinsi ya ku-

wainua wanawake katika nyanja zote, kuongeza nafasi za uongozi kwa wanawake, kutoa elimu bora kwa watoto wa kike na namna mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri haki za wanawake

Balozi Mulamula alisema katika ziara hiyo alipata nafasi ya kubadilishana mawazo na mawaziri mbalimbali kutoka nchi zingine sambamba na kupena ushauri katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni pamoja na kuwashawishi kuja kufanya uwekezaji Tanzania katika sekta za kilimo, utalii, usafiri wa anga pamoja na uchumi wa buluu.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na watumishi mbalimbali wa halmashauri na wilaya zote za Mkoa wa Mbeya katika kongamano la Nishati na Madini lililofanyika jijini humo, jana kwa lengo la kujadiliana namna ya kukuza sekta hiyo kwa kushirikiana na wachimbaji madini na wamiliki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

Wanafunzi 5,000 wasoma wakiketi chini Sengerema

Elizabeth Seleman, SENGEREMA

WANAFUNZI 5,000 kutoka shule za msingi wilayani Sengerema mkoani Mwanza, wanakaa sakafuni kutokana na kukabiliwa na uhaba wa madawati.

Ofisa Elimu wa shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Donaldi Bunonos, alibainisha hayo jana wakati akizungumzia hali ya miundombinu ya elimu kwa shule za msingi wilayani humo.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameagiza suala hilo limalizwe haraka.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi wilayani Sengerema walisema wanajisikia vibaya kusoma wakiwa wamekaa chini na kuiomba serikali iwasaidie kumaliza tatizo hilo.

Walisema wanashindwa kuanzisha vizuri kwani wanakuwa wanaandikia kwenye miguu, kitendo ambacho kinawafanya washindwe kuwa wasafi.

Baadhi ya wazazi waliomba serikali kulitazama tatizo hilo la ukosefu wa madawati kwa jicho la tatu kwa kuwa linawaathiri watoto kimasomo na kifya.

Wazazi walisema kuwa hawajawahi kushirikishwa katika suala zima la madawati shuleni.

Hivyo, waliomba serikali iwaruhusu wawanunulie madawati watoto wao wenyewe ili kila anavyoingia darasa lingine anakwenda nalo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Gabriel, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Nganga, kuhakikisha wanaweka mikakati ili kuwawezesha wanafunzi hao kusoma katika mazingira rafiki.



Ili kukabiliana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameagiza suala hilo limalizwe haraka.

Watoa tahadhari fursa mitandaoni

Na Beatrice Shayo

UMOJA wa Mashirika na Wadau wa Kupambana na Uhalifu katika Mtandao (ACCO) ume-washauri wananchi kuwa makini na fursa zinazotangazwa ili kuepuka kutapeliwa.

Mkurugenzi wa ACCO, Gretchen Peters, alitoa wito huo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao, kueleza kuwa kutokana na tatizo hilo wameandaa programu ili kusaidia kupunguza uhalifu huo.

Alisema tishio la uhalifu wa kimtandao kwa sasa hivi lime-shika kasi katika mitandao ya kijamii inayotumia lugha ya Kiswahili, hivyo wameamua kuja na programu ambayo itawasaidia vijana, wanafunzi na walimu kuepukana na tatizo hilo.

“Programu hii itashirikisha

vyombo vya habari katika kusaidia kuelimisha umma ili wawe salama wakati wanatumia mitandao. Kwa sasa kuna vijana wengi wa kitanzania ambao tayari wamejikuta katika tatizo hili,” alisema

Peters alisema Tanzania na nchi zingine za Afrika zina idadi kubwa ya matukio ya uhalifu wa kimtandao. Nchi kama Tanzania ina idadi kubwa ya vijana ambao kati yao wapo wanaanza kutumia mitandao ya kijamii kwa mara ya kwanza.

Mratibu wa ACCO Tanzania, Shubert Mwarabu, alisema wameungana kwa lengo la kukabiliana na uhalifu wa mtandao kutokana na kuwapo kwa shida kubwa katika mitandao na baadhi kutapelewa kwa simu janja.

Alisema kwa mujibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Aprili 2021, Tanzania ilikadiriwa kuwa na wa-

tumiaji wa mtandao takriban milioni 21.

Mwarabu alisema wananchi wengi wanahamasishwa kuingia mitandaoni kwa nia njema ama kuwasiliana na marafiki wakishirikiana katika fursa zilizopo mitandaoni, lakini tahadhari haijaweza kutolewa kwa watumiaji hao.

Alisema: “Watu wanaingia mitandaoni lakini zile tahadhari za upande wa uovu wa mtandao hazijazingatiwa jumuike hili la wadau. Alliance tumekuja pamoja kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi.”

Alisema suala la mtandao ni la kimtambuka, linahusu dunia nzima hivyo ni muhimu kuwapo kwa mikakati ambayo itamlinda mtumiaji.

“Kuna watu katika mtandao utawasikia wanasema wanatoa mikopo ndani ya saa 24 unaenda kujaza fomu kumbe

unatapeliwa.

“Pia kuna hizi fursa za ajira zinatangazwa hata nje ya nchi tunatakiwa kufahamu kuwa kupata kazi katika nchi za kigeni ni ngumu.

“Leo hii unakutana na mtu katika mtandao anakuambia unafaa kuwa mwana mitindo anakutengeza viza na tiketi unaenda mwisho wa siku unakutana na biashara haramu ya binadamu,” alitahadharisha.

Alisema fursa za mitandaoni zinatakiwa kila mmoja kijiridhisha kama zina ukweli ili kujilinda na matapeli.

Hivyo, aliipongeza serikali kutokana na kampeni mbalimbali ilizoanzisha ikiwamo sambaza mchongo siyo uongo iliyoratibiwa na TCRA na vyombo vya dola kupitia idara zake za uchunguzi wa kisayansi na usalama wa mtandao.

SBL KUENDELEA KUCHANGIA MAENDELEO YA MICHEZO

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha na kuchangia sekta ya michezo hapa nchini ambayo pia inaajiri Watanzania wengi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi wa mahusiano kwa umma wa SBL, Jonh Wanyancha Serengeti imekuwa ni mdau mkubwa wa maendeleo ya michezo na imekuwa ikifadhili michezo mbali mbali ikiwamo soka, riadha na mchezo wa gofu.

Alisema SBL inatambua

mchango wa michezo na kwamba kupitia chapa ya Serengeti imekuwa mstari wa mbele kuchangia maendeleo ya michezo.

Ni kupitia chini ya udhamini wa bia ya Serengeti Lager Timu ya Taifa (Taifa Stars) iliweza kufuzu mashindano makubwa kabisa barani Afrika (AFCON) yaliyofanyika nchini Misri mwaka 2019. Taifa Stars ilifuzu mashindano hayo ikiwa ni miaka 39 tangu ifuzu kwa mara ya mwisho.

Kabla ya kufuzu mashindano hayo makubwa barani Afrika, SBL kupitia kinywaji chake cha Serengeti Lager ilisaini mkataba wa miaka mitatu na

TFF ambapo ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kuidhamini.

Oktoba 2020 bia ya Serengeti Premium Lager (SPL) iliingia makubaliano na kusaini mkataba na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kwa ajili ya kuidhamini Taifa Stars kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Wakati wa kutiliana saini mkataba huo, rais wa TFF Wallace Karia alinukuliwa akisema SBL kupitia chapa ya Serengeti imekuwa ni mfano wa kuigwa katika kuchangia maendeleo ya michezo na

kuyataka makampuni mengine kuiga mfano.

Mkataba huo unaogharimu shilingi bilioni 3 za Kitanzania, umesainiwa baada ya ule wa awali uliosainiwa mwaka 2017, kufikia ukomo kati kati ya mwaka huu huku timu ikijivunia mafanikio mengi katika kipindi cha udhamini.

SBL kupitia bia ya Serengeti Lite pia imekuwa mdau mkubwa wa soka la wanawake. Serengeti Lite ndiyo mdhamini wa kwanza na wa pekee kwa ligi ya wanawake tangu ianzishwe hapa nchini. SBL pia imekuwa ikisaidia michezo mingine ikiwamo Gofu na riadha.



Wachezaji Simba Queens wakishangilia na Kombe lao la ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara msimu huu 2021/2022, baada ya kukabidhiwa. **PICHA: SIMBA**

Kocha kuamua hatima ya Kichuya Namungo

Na Saada Akida

MWENYEKITI wa timu ya Namungo FC, Hassan Zidada amesema hatma ya kuwaongeza mkataba nyota wao wawili, Shiza Kichuya na kipa Jonathan Nahimana iko chini ya kocha wao Hanoor Janza.

Mikataba ya wachezaji hao imefikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu

Tanzania bara jana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zidada alisema baada ya kumalizika kwa mchezo na Mbeya City jana wanatarajia kukutana na kocha huyo kwa ajili ya kupitia tathimini ya timu hiyo kwa msimu huu uliofikia tamati.

Alisema kikao hicho kitajadili hasa suala la wachezaji ambao wataongezewa mkataba

ikiwemo Kichuya na Hitimana na wachezaji wengine ambao mchango wao unahitajika.

"Ni kweli kuna baadhi ya wachezaji ikiwemo huyo na wengine, suala hilo liko mikononi mwa kocha wetu kuangalia kama tutawaongeza mkataba au la, bado wachezaji wazuri na kama viongozi tunahitaji kupata mchango wa nyota hao," alisema Zidada.

Alisema hawakufanya vizuri msimu huu wa Ligi hali ambayo wanatarajia kukutana na kocha huyo kujadiliana mambo mbalimbali kwa msimu ujao.

"Mbali na usajili lakini pia tunahitaji kukutana naye tujue hatma ya kocha wetu huyo ikiwemo kuendelea kubaki nasi kwa msimu ujao wa Ligi," alisema Zidada.

Timu ya taifa ya tenis kupaa Uganda

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya Taifa yenye wachezaji watano ya mchezo wa tenis inatarajiwa kuondoka nchini Julai 2 mwaka huu kuelekea Uganda kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia yatakayoanza kutimua vumbi Julai 4. Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Chama cha tenis Tanzania (TTA), Denis Makoi alisema wachezaji watatu wanatoka mkoani Arusha na wawili wanatoka Dar es Salaam.

Alisema maandalizi yanaendelea vizuri na wamewaweka kambini wachezaji wao kipindi kirefu ili wakaiwakilisha vema nchi.

"Kwa upande wetu maandalizi yamekamili kwa asilimia mia moja kila mchezaji ana morali ya kwenda kufanya vizuri," alisema Makoi.

Alisema kutokana na maandalizi wanayopewa wachezaji hao wakiwa chini ya Kocha wao mkuu Salum Mvita yatawasadia kupata matokeo mazuri.

Naye Kocha mkuu wa timu hiyo Salum Mvita alisema anaendelea kuwanoa wachezaji wake kuelekea kwenye michuano hiyo.

Wasisitizwa kujitokeza Tamasha la Utamaduni

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ametoa wito kwa Wananchi kujitokeza na kushiriki katika Tamasha la Utamaduni la kwanza kitaifa na Siku ya Kiswahili Duniani linalotarajiwa kuanza Julai mosi hadi saba jijini humo.

Akizungumza jana wakati akitoa taarifa juu ya tamasha hilo, alisema wanatarajia lithahudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia alisema tamasha hilo litazinduliwa Julai 02 na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwenye Uwanja wa Uhuru, huku likihusisha matembezi ya utamaduni, maonyesho ya vyakula vya asili na ngoma za asili.

"Julai tatu kutakuwa na Usiku wa Taarabu katika ufukwe wa Coco Beach ukihusisha burudani ya muziki mwanana kutoka kwa wasanii mbalimbali akiwemo Khadija Kopa, Isha Mashauzi, Patricia Hilary, Mzee Yusuph na vikundi na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson," alisema Makalla.

Aliongeza kuwa Julai nne kutakuwa na maandamano ya amani kuhusu lugha ya Kiswahili na utoaji haki kutoka Temeke mwisho mpaka Uwanja wa Uhuru ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro.

Vile vile alibainisha kuwa Julai sita kutakuwa na kongamano la mchango wa lugha ya Kiswahili katika harakati za ukombozi wa bara la Afrika likihusisha Viongozi kutoka ndani na nje ya nchi.

Aidha, alieleza kuwa Julai saba Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Siku ya Kiswahili Duniani ambayo itaadhimishwa kwa mara ya kwanza duniani, huku akisisitiza wananchi kujitokeza kwa wingi siku hiyo.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

RAPHINA ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inakaribia kuafikiana na Leeds kuhusu dau la kumnunua mshambuliaji wa Brazil na Leeds United, Raphina, 25, ambaye pia anazivutia klabu kama vile Arsenal na Barcelona (**Guardian**)

SKRINIAR AGOMBEWA

CHELSEA sasa imebadilisha mawazo yake na inamnyatia beki wa AC Milan na Slovakia, 27, Milan Skriniar ambaye pia analengwa na PSG baada ya kubaini kwamba kifungu cha kumuuzwa mchezaji wa Juventus na Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22 ni ghali mno. (**Mail**)

PSG KUZOA NYOTA

KLABU ya PSG imekubaliana maslahi binafsi na Milan Skriniar pamoja na kiungo wa kati wa Lille na Ureno, Renato Sanchez mwenye umri wa miaka 24. (**Get French Football News**)

WATANO WATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imehusishwa na harakati za kumnunua mchezaji mwingine wa tatu wa klabu ya Manchester City. The Blues inataka kumnunua mshambuliaji wa Ukraine, Oleksandr Zinchenko, 25, kutoka kwa mabingwa hao wa ligi Kuu England. (**Mail**)

ERIKSEN KUSHAWISHIWA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anatumaini kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, kutamshawishi kiungo mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30 kujiunga na klabu hiyo ya Old Trafford. (**Star**)

SPURS NA RICHARLISON

KLABU ya Tottenham Hotspur imeimarisha harakati zake za kutaka kumsajili mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison, 25, lakini ombi la pauni milioni 20 ambalo lilishirikisha winga wa Uholanzi Steven Bergwijn mwenye miaka 24, limekataliwa na Toffees hao. (**Telegraph**)

SPENCE KWENDA FOREST

KLABU ya Middlesbrough imekasirishwa na hatua ya klabu ya Tottenham Hotspur kusitisha makubaliano ya kumnunua beki wa kulia wa England, Djed Spence, 21, na hilo linaweza kufungua milango ya Nottingham Forest kumnunua mchezaji huyo. (**Football League World**)

DOUCOURE KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Lens, Cheick Doucoure, 21, katika makubaliano yenye thamani ya euro milioni 21 pamoja na marupurupu kwa mchezaji huyo wa Mali. (**Guardian**)

PEREIRA KUBAKI FLAMENGO

FULHAM imeruhusiwa kuzungumza na kiungo wa kati wa Brazil, Andreas Pereira, 26, baada ya kukubaliana dau na Manchester United, ijapokuwa mchezaji huyo anataka kubakia katika timu ya Flamengo ya nchini Brazil ambapo yupo kwa mkopo. (**90 Min**)

BROWNHILL ATAKIWA

KLABU ya Southampton imejiunga kwenye mboja za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Burnley na England, Josh Brownhill, 26. (**90 Min**)

DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



NEYMAR AITWA CHELSEA

LONDON, England

THIAGO Silva amemsihi mchezaji mwenzake wa Brazil, Neymar ajitunge naye kule Chelsea ikiwa ataamua kuondoka pale Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa BBC Sport.

Hivi karibuni kumeibuka uvumi kuhusu mustakabali wa Neymar pale PSG, huku klabu hiyo ya Ufaransa ikiripotiwa kuwa tayari kumuuzwa iwapo dau linalokubalika litapatikana.

Wakala wa zamani wa Neymar,

●●● Ni kama akitaka kuondoka PSG, wakala wake asema anataka kushinda kwanza...

Wagner Ribeiro alisema wiki iliyopita mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 anataka kubaki PSG, ili kutimiza ndoto yake ya kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Na sasa beki wa Chelsea, Thiago Silva mwenye umri wa miaka 37, ambaye alicheza pamoja na Neymar katika ngazi ya kimataifa na PSG kutoka mwaka 2017 hadi 2020,

ametaka kuungana naye pale Stamford Bridge.

"Lazima aende Chelsea," alisema Silva akiambia Globo na kunukuliwa na BBC Sport kuhusu Neymar ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2025.

"Iwapo anakaribia kuondoka, basi lazima aende huko Chelsea. Ikitokea, basi matarajio ni bora zaidi."

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- **1,010,68**

MECHI KALI

KLUBI 04

VERSUS

LLVES 2

1 | **1.39**

X | **4.89**

2 | **5.68**

LINGARD KURUDI WEST HAM

LONDON, England


KOCHA wa West Ham United, David Moyes anashinikiza klabu hiyo kumnunua tena Jesse Lingard kwa uhamisho wa bure, kwa mujibu wa 90min.

Wagonga nyundo hao tayari wamekuwa na shughuli nyingi kwenye dirisha la usajili la majira haya ya joto, wakiwaleta Nayef Aguerd na Alphonse Areola kutoka Rennes na Paris Saint-Germain, lakini wanataka kusajili angalau wachezaji wengine wanne au watano ili kuhakikisha wanashindana katika Ligi Kuu ya England na Ligi ya Europa Conference.

Lingard anakaribia kuwa mchezaji huru baada ya Manchester United kuchagua kutoongeza mkataba wake pale Old Trafford, na analengwa kwa muda mrefu na West Ham - kutokana na msimu wa mkopo uliofanikiwa msimu wa 2020/21 na kufikisha mabao tisa katika mechi 16.

West Ham ilijaribu kumsajili Lingard kwa mkataba wa kudumu msimu uliopita wa joto - ingawa alichagua wakati huo kusalia Old Trafford na kupigania nafasi yake.

Vyanzo sasa vimeithibitishia 90min kwamba, Moyes, ambaye amem-sifu Lingard hadharani mara kadhaa, anaendelea kushinikiza uongozi wa West Ham kufikia makubaliano, na ana matumaini ya matokeo mazuri.



Pauni mil 65 kwa Raphinha

LONDON, England

KLABU ya Chelsea imeibuka kama ndiyo yenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili winga wa Leeds United, Raphinha baada ya kutoa ofa ya pauni milioni 65 ikijumuisha nyongeza kwa mchezaji mmoja kwa ajili ya nyota huyo wa kimataifa wa Brazil.

The Blues tayari walikuwa wakifuatilia hali ya mchezaji huyo na ghafla wamepiga hatua mbele kwenye mbio hizo, ambazo pia zipo Barcelona na Arsenal.

Barcelona pamekuwa mahali anapopendelea Raphinha hadi sasa, lakini mtandao wa 90min umefichua kwamba, Wakatalunya

hao wanakabiliwa na ukata. Fedha zimesalia kuwa wasiwasi kwa klabu hiyo ya Hispania kuhusu uhamisho wa msimu huu wa joto na biashara itategemea mauzo ya wachezaji wengine.

Awali iliilezwa kuwa Arsenal pia walikuwa wame-wasilisha ofa kwa Mbrasil huyo katika jaribio la kutaka kumsajili, lakini ofa hiyo haikufikia hesabu ya Leeds na ikakataliwa mara moja.

Washikabundi sasa wanafikiria iwapo wangeze ofa

yao kwa kuzingatia uhamisho wa Chelsea.

Raphinha alifanikiwa kufunga mabao 11 na kutoa pasi tatu za mabao kwenye Ligi Kuu England msimu uliopita, ingawa Leeds walikuwa wakipigana katika matokeo mabaya.



KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.



SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588



@TZSportPesa



@SportPesaTZ



@tzsportpesa

HABARI MICHEZO

89,585/-

KOCHA MPYA SIMBA APEWA MASHARTI

Na Waandishi Wetu

KLABU ya Simba ambayo juzi usiku imemtangaza kocha mpya mwenye uraia pacha wa Serbia na Ureno, Zoran Manojlovic, imesema imempa malengo ya kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kurudisha mataji yote mawili iliyopokonywa, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Kluba hiyo, Ahmed Ally, amesema pamoja na wasifu mzuri wa kocha huyo, lakini kili-chowavutia zaidi ni rekodi yake ya kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika akiwa na timu ya Primeiro de Agosto ya Angola.

“Ana wasifu (CV) nzuri sana nzuri sana, tumevutiwa na uzoefu wake hasa

kwenye soka la bara la Afrika, amefundisha Kusini mwa Afrika, Kaskazini na Kati, na kikubwa zaidi ni kuifikisha timu ya Angola kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa, na hilo ndilo sisi tunahitaji zaidi,” alisema Meneja Habari huyo.

“Tumempa malengo yetu kwa kumwambia kuwa tunaitaka nusu fainali ya CAF na mataji yetu yote mawili ya Ligi Kuu na Kombe la FA yarejee Msimbazi.”

Kocha huyo alifikisha Primeiro de Agosto hatua ya nusu fainali mwaka 2018.

Mbali na timu hiyo ambayo aliifundisha kuanzia mwaka 2017 hadi 2019, pia alizifundisha timu za Wydad Casablanca ya Morocco, 2019 hadi 2020, kabla ya kuhamia Al Hilal ya Sudan 2020 hadi 2021, na baada ya hapo akaenda nchini Algeria kuifundisha CR Belouizdad mwaka jana, lakini hakukaa sana akaenda kujiunga na Al Tai ya Saudi Arabia.

Alisema wamempa mwaka mmoja ambao pia una kipengele cha kuongeza mkataba kama akifanya vizuri ndani ya

muda huo.

“Ni mwaka mmoja, haya ni maamuzi ya kiutawala, ila ni mwaka mmoja wenyewe nafasi ya kuongeza kama akifanya vizuri. Akifanya vile ambavyo tunakusudia tutamwongeza mkataba kwa hiyo wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi na kujiuliza kwa nini wamempa mwaka mmoja, kocha unaweza kumpa miaka mitano, halafu akakaa miezi mitatu au sita unaweza kumtimua, inategemea na matokeo ya timu,” alisema.

Alisema kwa sasa kocha anafanya kazi kwa karibu na viongozi kwa mfumo wa mawasiliano ya kisasa, kabla ya kukabidhiwa timu kuiandaa kwa maandalizi ya msimu ujao.

“Kocha atawasili moja kwa moja, timu itapoanza maandalizi ya msimu unaokuja, yeye atasalia huko huko akiendelea kufanya kazi na viongozi kwa njia za kisasa na timu ikikamilika atakabidhiwa aende nayo kwenye maandalizi ya msimu akaitengeneze ili tukirejea aje auwashe moto,” alisema kwa majigambo.



Waziri wa Afya, Ummu Mwalimu akimkabidhi cheti cha utambuzi Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Child Help Tanzania (CHT), Hakim Bayakub, baada ya kuhitimisha mbio za marathon kwa ajili ya kuchangia fedha za matibabu kwa watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, zilizoandaliwa na Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI). CHT ni moja ya taasisi zilizofadhili mbio hizo. **PICHA: MPIOGAPICHA WETU**

Ummu aongoza marathon ya kuchangia watoto 200

Na Sabato Kasika

WAZIRI wa Afya, Ummu Mwalimu, amewataka waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha madini ya foloki asidi yanapatika kwa urahisi katika ngazi zote za kutolea huduma za afya hadi zahanati.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki baada kushiriki mbio za marathon na watoto wenye ulemavu huo, zilizoandaliwa na Taasisi ya Mifupa (MOI) kwa ajili ya kuchangisha fedha za matibabu kwa watoto 200 wenye ulemavu huo.

Mbio hizo zilifanyika jijini Dar es Salaam, huku akifafanua kuwa tatizo la watoto kuzaliwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi linaweza kuzuilika, kwa kuwa linatokana na ukosefu wa foliki asidi.

Alisema, watoto wanaozaliwa na changamoto ya kichwa kikubwa na mgongo wazi bado ni tatizo nchini, na kwamba takwimu zinaonyesha katika nchi tano barani Afrika zenye watoto wengi wanaozaliwa na changamoto hiyo, Tanzania inashika namba tatu ikiwa imetanguliwa na Algeria na Ethiopia.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya MOI, Prof. Charles Mkony amemshukuru waziri kwa kushiriki mbio hizo na kuendelea kuiunga mkono taasisi hiyo kwa kutoa huduma bora kwa Watanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema, kupitia fedha ambazo wamewahi kuchangisha na kuweka kambi ya huduma za matibabu, tayari watoto 20 walishapata huduma hiyo.

SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

TAREHE	MUDA	MICHEZO	NYUMBANI SARE UGENINI		
			1	X	2
2.7.2022	22:00	Ituano SP vs Criciuma SC	2.41	2.93	3.18
2.7.2022	22:30	Fluminense vs Corinthians	2.23	3.04	3.48
3.7.2022	01:00	Santos vs Flamengo	2.84	3.14	2.54
3.7.2022	01:00	Ceara CE vs Internacional	2.49	3.04	2.99
3.7.2022	02:30	Toronto vs Seattle Sounders	2.65	3.75	2.43
3.7.2022	02:30	CRB AL vs Guarani SP	2.39	2.82	3.37
3.7.2022	02:30	Gimnasia y Esgrima vs Defensa Justicia	2.27	3.39	3.19
3.7.2022	13:30	Suwon Samsung vs Incheon Utd	2.49	3.19	2.89
3.7.2022	16:00	Varbergs Bois vs IFK Varnamo	2.49	3.15	2.90
3.7.2022	16:00	Djurgardens IF vs Hammarby	2.23	3.42	3.08
3.7.2022	18:00	Danubio FC vs River Plate (URU)	2.52	3.16	2.81
3.7.2022	18:30	BK Hacken vs Elfsborg	2.41	3.52	2.73
3.7.2022	19:00	Union Santa Fe vs Lanus	2.25	3.20	3.30
3.7.2022	19:00	Aalesunds vs Stromsgodset	2.24	3.47	3.02
3.7.2022	21:00	Barracas Central vs San Lorenzo	2.90	3.15	2.50
3.7.2022	22:00	Atletico GO vs Sao Paulo	2.99	3.04	2.48
3.7.2022	22:00	Bahia BA vs Gremio	2.63	2.78	3.03

MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 30/06/2022

12:00	3445	Sparta Prague vs Opava	1.33	5.08	6.64
12:00	4357	Kaya FC vs Bali Utd Pusam	5.89	4.71	1.39
12:30	2396	Guangzhou Evergrande vs Wuhan Three Towns FC	34.40	9.83	1.03
13:00	1659	Sebeta City FC vs Arba Minch Kenema	3.53	2.85	2.15
14:30	2230	Hebei Zhongji vs Wuhan Zall	8.82	4.80	1.28
14:30	5687	Beijing Guoan vs Chengdu Qianbao	2.06	3.19	3.33
14:30	5789	Shanghai Jiading Hulong vs Beijing BG	3.48	3.18	2.01
16:00	2381	Banfield Reserva vs Boca Jrs	3.04	3.28	2.15
16:00	4463	Sidama Buna SC vs Hadiya Hosahina FC	2.40	2.90	2.95
16:00	5066	Italy W U19 vs France W U19	4.50	3.75	1.70
17:00	1652	Estudiantes de LP Reserve vs Arsenal FC Reserve	1.77	3.50	4.30
17:00	3255	Phnom Penh vs Young Elephants FC	1.62	3.90	4.90
17:00	4536	Metallurg Bekabad vs Lokomotiv Tashkent	2.60	2.80	2.80
17:00	4860	CA Lanus vs CA Union Santa Fe Reserve	1.98	3.38	3.34
18:00	1893	Jazeera Amman vs Moghayer AL Sarhan	2.85	3.34	2.22
18:00	2255	Eding Sport FC vs Canon Sportif	2.56	3.00	2.66
18:00	2803	Nasaf Qarshi vs FC Olimpik	1.37	3.89	8.87
18:00	4123	FCI Levadia Tallinn U21 vs Flora II	1.40	3.89	2.53
18:00	4310	Valmiera FK/Bjss vs Spartaks Jurmala	1.08	8.04	20.59
18:30	2394	Bouake FC vs FC San Pedro	5.11	2.80	1.83
18:30	3183	Czech Republic W U19 vs Spain W U19	24.49	14.69	1.01
18:30	5793	Klubi 04 vs Ilves 2	1.39	4.89	5.68
19:00	1937	Paide Linnameeskond vs FC Elva	1.34	5.66	6.67
19:00	2429	Ullensaker/Kisa vs Ranheim	2.94	3.68	2.05
19:00	2686	Parnu Jalgpalliklubi vs Harju JK Laagri	10.12	6.48	1.22
19:00	3321	Viljandi Tulevik-Ida vs Virumaa FC Alliance	4.15	4.05	1.72
19:00	3343	Switzerland W vs England W	8.66	4.92	1.28
19:00	3589	Rigas Futbola Skola vs BFC Daugavpils	1.19	6.08	10.79
19:00	3698	Sandnes Ulf vs Rosenborg	5.10	4.22	1.50
19:00	3864	Viimsi JK vs FC Nomme United	1.46	4.96	5.47
19:00	4769	Brann vs Fredrikstad	1.32	4.91	7.07
19:00	5310	Kfum Oslo vs Sogndal	2.16	3.38	2.94
19:00	5498	Melhus vs Rosenborg BK 2	3.04	4.61	1.80
19:30	1415	Riteriai B vs FA Siauliai B	3.09	3.53	2.03
20:00	2356	Piteaa IF vs Tegs SK	1.35	4.71	6.68
20:00	4917	CSKA Pampir Dushanbe vs FK Neftchi Kochkor-Ata	1.62	4.10	4.60
20:00	5442	Angelholms vs Tvaakers IF	2.40	4.11	2.27
20:30	1788	Wihdat Amman vs Al Sareeh	1.61	3.74	4.72
20:30	3914	Rappe Goif vs FC Rosengard	2.69	3.67	2.19
21:00	3062	Thor Akureyri vs Throttur Vogum	1.60	3.94	4.54
21:30	4423	Fjolnir vs HK Kopavogs	2.40	3.68	2.42
22:30	1326	Societe Omnisport vs ASEC Mimosas	5.20	3.20	1.75
23:00	1340	Vaengir Jupiters vs Kari	2.23	4.22	2.41
23:30	5880	Aragua FC vs Metropolitanos	3.20	2.80	2.32

IJUMAA - 01/07/2022

01:00	3012	America Mineiro MG vs Botafogo RJ	2.03	3.04	3.58
01:15	2028	Independiente DV vs Lanus	1.64	3.59	4.72
01:30	2134	HFX Wanderers FC vs Atletico Ottawa	2.45	3.10	2.71
02:00	3378	Charlottes FC vs Austin FC	2.23	3.46	3.10
02:00	4950	Nublense vs Audax Italiano	1.75	3.49	4.13

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Yanga bingwa bila kupoteza

●●● Mpole mfungaji bora, Biashara yashuka, Mtibwa vs Prisons 'Play off'...

Na Adam Fungamwango

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2021/22 ilimalizika rasmi jana kwenye viwanja mbalimbali nchini, huku ikishuhudia Mabingwa wapya, Yanga, wakiweka rekodi ya kumaliza msimu bila kupoteza mechi yoyote baada ya kuifunga Mtibwa Sugar bao 1-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku Biashara United ikiifuata Mbeya Kwanza kushuka daraja na kwenda Championship.

Wakati Yanga ikimaliza ligi na pointi 74, bila kupoteza kama zilivyowahi kufanya Simba mwaka 2009/10, na Azam 2013/14, straiika wa Geita Gold, George Mpole amefanikiwa kutwaa kiatu cha dhahabu baada ya jana kufunga bao lake la 17 kwenye mechi ya mwisho dhidi ya Coastal, Union timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga huku bao la wenyeji likifungwa na Rashid Chambo.

Mpole amempiku straiika wa Yanga, Fiston Mayele aliyemaliza na mabao 16, ambaye pamoja na kuhangaika huku na huko jana, aliambulia patupu, akibanwa vilivyo na mabeki wa Mtibwa Sugar.

Yanga ilipata bao pekee kwenye mchezo huo dakika nane kabla ya mechi kumalizika likifungwa na mchezaji mdogo kuliko wote kwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, mwenye miaka 19, Denis Nkane.

Azam FC, imefanikiwa kukata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Barani Afrika, baada ya ushindi mnono wa mabao 4-1 dhidi ya Biashara United na kuitumbukiza kwenye shimo la kushuka daraja.

Yalikuwa ni mabao matatu ya Mkomani Idriss Mbombo na Never Tegere, huku Gershon Kabeja akiifungia Biashara bao la kufutia machozi.

Ni ushindi ulioibakisha Azam kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi 49 na kuiacha Geita Gold kwenye nafasi ya nne kwa pointi 46.

Mbombo amefunga mabao matatu kwenye mechi moja na kutimiza 'hat-trick' tatu kwenye Ligi Kuu msimu huu,

zingine zikiwa ni za Jeremiah Juma wa Prisons, na Shiza Kichuya wa Namungo.

Timu za Mtibwa Sugar na Prisons ndizo zitakazokwenda kucheza mechi za mchujo baada ya kushika nafasi ya 13 na 14.

Baada ya kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga, Mtibwa inakuwa kwenye nafasi ya 13 na pointi zake 31, huku Prisons baada ya kudunguliwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting imeachwa kwenye nafasi ya 14, ikiwa na pointi 29.

Ni ushindi ulioinusu ruvu Shooting kucheza mechi ya mchujo.

Timu hizo sasa zitalazimika kucheza mechi mbili za 'play off' nyumbani na ugenini, na timu itakayokuwa mshindi wa jumla, itabaki Ligi Kuu, na itakayofungwa itakwenda kucheza mechi nyingine ya nchujo na timu kutoka Ligi ya Championship ambayo tayari imeshapatikana, JKT Tanzania.

Yoyote itakayocheza na JKT Tanzania mechi za nyumbani na ugenini, ikishinda itabaki Ligi Kuu, lakini ikifungwa itashuka daraja na kwenda Championship na kuwapisha JKT Tanzania ambao wakishinda wanapata.

Simba iliyoutema ubingwa msimu huu baada ya kukaa nao kwa misimu minne, ilimaliza ligi kwa suluhu dhidi ya timu ambayo imeshashuka daraja, Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea, Ruvuma.

Dodoma Jiji ikiwa nyumbani, Uwanja wa Jamhuri, iliichapa KMC bao 1-0 lililofungwa na Waziri Junior, Kagera Sugar ikitoka suluhu dhidi ya Polisi Tanzania, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, Mbeya City ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo.

MPOLE AMSHUKURU MUNGU

Mara baada ya kuibuka mfungaji bora kwenye Ligi hiyo akiwa na mabao 17, Mpole amemshukuru Mwenyezi Mungu kwa kulifanikisha hilo.

Kupitia ukurasa wake wa facebook, Mpole aliandika: "Asante Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kutwaa kiatu cha dhahabu cha Ufungaji bora.

"Haikuwa rahisi, lakini nimefanikiwa. Asanteni pia mashabiki ambao mmekuwa pamoja na mimi kwa kipindi chote hiki."

Mpole alifunga bao hilo kwenye mchezo dhidi ya Coastal Union ambao ulimalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1.

Na sasa hiyo ilimfanya kumzidi mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele kwa bao moja.



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Mtibwa Sugar, Oscar Masai wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara baina ya timu hizo jana kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: YANGA**

Raphinha atakiwa kwa pauni mil 65

LONDON, England

KLABU ya Chelsea imeibuka kama ndiyo yenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili winga wa Leeds United, Raphinha baada ya...

HABARI UKURASA. 22



Lingard kurudi West Ham

LONDON, England

KOCHA wa West Ham United, David Moyes anashinikiza klabu hiyo kumnunua tena Jesse Lingard...



HABARI UKURASA. 22



9 770856 541002 >